

RITA KUMALIZA MIGOGORO YA MIRATHI INAYOJITOKEZA MARA KWA MARA KATIKA JAMII.

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) unakusudia kupitia upya sheria ya mirathi katika eneo la Wakfu ili kuona uwezekano wa kuanzishwa kwa kamisheni ya Wakfu chini ya Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu itakayokuwa na jukumu la kushughulikia masuala yote yanayohusu mirathi.

Hayo yameelezwa hii leo Jijini Dar es salaam na Mkurugenzi wa ulinzi wa haki za kisheria kutoka RITA Bi Lina Msanga wakati wa kufunga mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa kwa kushirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar kuhusu usimamizi na kushughulikia migogoro ya mirathi pindi itakapotokea warithi kutokuelewana.

Bi Msanga ameongeza kuwa, Wakala utawasiliana na Wizara ya katiba na sheria kuona namna bora ya kuanzisha Kamisheni ya Wakfu na uratibu wa masuala ya Hijja kama inavyofanyika kwa upande wa Zanzibar.

Kwa upande wake Mwanasheria wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar Bw Assaa Jaffar Omar amesema kuwa kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa kumaliza migogoro ya mirathi kutokana na sheria iliyopo kukipa nguvu na mamlaka chombo hicho ya kusimamia masuala yote yanayohusu Wakfu na Mali ya amana pamoja na elimu wanayoendelea kuitoa kwa jamii kuhusu mgawanyo wa mirathi kwa njia ya sharia na sheria za Nchi.

Akizungumzia uzoefu wao katika kushughulikia migogoro ya mirathi za Kiislam Mkuu wa Urithi Kamisheni ya Wakfu Zanzibar Bw Haji Mussa Khatib ameeleza kuwa ofisi yake imeweka utaratibu wa kufanya mawasiliano ya moja kwa moja na Ofisi ya Mufti, Mahakama ya Kadhi na Mahakama za Zanzibar ambapo wanafanya kazi kwa kushirikiana na hivyo kupelekea mirathi nyingi kufungwa kwa wakati bila ya kutokea migongano baina ya wanandugu na vyombo vingine vinavyosimamia haki.

Mbali na mafunzo hayo RITA na Kamisheni ya Wakfu Zanzibar kwa pamoja wamekubaliana kubadilishana uzoefu kila baada ya miezi sita huku kukiwekwa maazimio kumi na moja (11) yenye lengo la kukuza ushirikiano na kufanya kazi kwa pamoja hasa kwa kuzingatia mafungamano yaliyopo kati ya Wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara.